JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE

5 JULAI, 2010

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE – TAREHE 5 JULAI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha

2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:

166. MHESHIMIWA STEPHEN JONES GALINOMA (KALENGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa takwimu ya watumishi wa Serikali Kuu kwa upande mmoja na Serikali za Mitaa kwa upande mwingine hadi kufikia tarehe 31/12/2009;

(b) Je, kulikuwa na watumishi hewa wangapi, na Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kumaliza tatizo hilo.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

167. MHESHIMIWA YONO STANLEY KEVELA (NJOMBE MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa:- Mashirika ya **COMESA, SADC** na Jumuiya ya Afrika Mashariki **(EAC)** ni vyombo muhimu sana kiuchumi na kisiasa, lakini vyombo hivyo vina mgawanyiko mkubwa sana wa kiuwanachama kama vile Tanzania kuwa

mwanachama wa **SADC** na Kenya na Uganda kuwa wanachama wa **COMESA**:-

(a) Je, Serikali za nchi hizo zina mpango gani wa kuondoa tofauti zilizopo;

(b) Je, kuna faida gani ambazo Tanzania inazipata kutokana na kujiunga na **SADC.**

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:

168. MHESHIMIWA AME PANDU AME (NUNGWI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Vigezo vyote vinavyotakiwa ili kuweka Tawi la Benki vipo mjini Nungwi – Tanzania Zanzibar:-

Je, ni lini Serikali itafungua Tawi la Benki ya **NMB** au **CRDB** huko Nungwi Zanzibar ambako ni kitovu cha utalii, biashara mbalimbali, hoteli n.k. na kwamba kutokuwepo kwa huduma hiyo ya Kibenki kunawasababishia wananchi usumbufu mkubwa.

169. MHESHIMIWA HERBERT JAMES MNTANGI (MUHEZA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Majukumu makubwa ya Mipango ya Maendeleo kwa wananchi yamewekwa chini ya Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Jiji na hivyo Wizara kubaki na majukumu ya kuandaa sera na usimamizi:-

Je, ni kwa nini katika Mfumo wa Bajeti, bado Wizara zinatengewa fedha nyingi za Utawala na Uendeshaji wa Idara mbalimbali wakati Halmashauri zinapata mafungu madogo ya mishahara ya Watendaji na utekelezaji wa mipango michache ya maendeleo.

WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

170. MHESHIMIWA PAUL PETER KIMITI (SUMBAWANGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Serikali imejitahidi sana kununua Mahindi katika msimu huu kwa ajili ya Ghala letu la Taifa la Hifadhi ya Chakula lakini bado baadhi ya Mahindi ya msimu uliopita hayajanunuliwa yote Mkoani Rukwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusomba Mahindi yote toka Maghala ya Sumbawanga, Songea na Makambako ili yapelekwe kwenye masoko ya Dar es Salaam na Dodoma ili kutoa nafasi kwa Mahindi ya msimu huu;

(b) Mwaka huu Mkoa wa Rukwa unatarajia kuvuna tani nyingi za mahindi; Je, kwa nini Serikali isianze

kuandaa magunia na dawa za kuhifadhia Mahindi ili kuwa na maandalizi mazuri kuliko msimu uliopita.

171. MHESHIMIWA SALIM HEMED KHAMIS (CHAMBANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Serikali ilipojibu Swali la Mhe. Lucy Mayenga katika Mkutano wa Kumi na Nane ilisema kuwa, upungufu wa nafaka ulifikia tani 1,348,445 mwaka 2009, na kutokana na hali hiyo Serikali ikasitisha uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi, lakini mwezi Februari, 2010 imeripotiwa na vyombo vya habari kuwa, kuna zaidi ya tani 500 za Mpunga wenye thamani ya zaidi ya shs.milioni 800 kwenye maghala huko Mbarali zikisubiri soko:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, haikufanya utafiti wa kutosha kabla ya kueleza hali ya chakula nchini;

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kuendelea kumzuia mkulima asiuze mazao yake nje ya nchi kunaongeza umasikini na kudumaza maendeleo ya mkulima wa Tanzania.

172. MHESHIMIWA JANET BINA KAHAMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Zipo taarifa kutoka Shirika la Vyama vya Ushirika la Tanzania **(T.F.C)** kwamba, Mchakato Mzima wa kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika iliyopendekezwa katika Mpango Kabambe wa Mwaka 2005 wa kuboresha tija na ufanisi katika mfumo wa Vyama vya Ushirika ili uendane na mtindo wa kisasa kwa kuendesha biashara ulikamilika Mwaka 2009, na taarifa rasmi kutolewa kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika:-

(a) Je, kama hivyo ndivyo, ni vikwazo gani ambavyo vinachelewesha uanzishwaji wa Benki hiyo muhimu,

(b) Je, Serikali inatambua kwamba kuwepo kwa Benki ya Taifa ya Ushirika ni muhimu kwa Maendeleo na uhai wa Ushirika nchini na hasa kutokana na

mzigo mkubwa unaobebeshwa Vyama vya Ushirika kutokana na masharti magumu yatolewayo na Benki za Biashara kwa Vyama vya Ushirika.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

173. MHESHIMIWA MAGDALENA HAMIS SAKAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Serikali imekuwa ikihamasisha Vyuo Vikuu hapa nchini kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kujiunga na masomo ya Vyuo Vikuu lakini ndani ya muda mfupi idadi hiyo imeongezeka kwa zaidi ya asilimia mia moja (100%) kwa lengo la kutoa fursa zaidi kwa vijana Watanzania kupata elimu ya juu:-

Je, Serikali ina mipango gani madhubuti ya kupanua miundombinu ya Vyuo hivyo kama vile Madarasa, Maktaba, Maabara, Hosteli n.k ili kukidhi mahitaji ya idadi kubwa ya wanafunzi wanaoongezeka kila mwaka.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

174. MHESHIMIWA DK. CHARLES OGESA MLINGWA (SHINYANGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Huduma ya maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga Mjini inasimamiwa na Mamlaka mbili za **KASHWASA** na **SHUWASA**:-

(a) Je, ni nini uhusiano wa Mamlaka hizo katika kutoa huduma bora ya maji katika Mji wa Shinyanga;

(b) Je, ni matatizo gani yaliyojitokeza mpaka sasa katika kutoa huduma ya maji chini ya Mamlaka mbili.

175. MHESHIMIWA GODFREY WESTON ZAMBI (MBOZI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Serikali ilikubali ombi la wananchi wa Mbozi hasa wa Kata za Mlangali, Iyula, Ruanda na Muyovizi kuwapatia maji kupitia Mradi wa Maji "Lukululu Group":-

Je, mradi huo umefikia wapi na unategemewa kukamilika lini.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

DODOMA **DKT. T.D. KASHILILAH**
5 JULAI, 2010 **KATIBU WA BUNGE**